

③ Kwa maana Kristo naye aliteswa mara moja kwa ajili ya dhambi, mwenye haki kwa ajili yao wasio haki, ili atulete kwa Mungu; mwili wake akauawa, bali roho yake akahuishwa. **1 Petro 3:18.**

4 BWANA YESU AWEZA KUOKOA NA KUHIFADHI.

① Naye, kwa sababu hii, aweza kuwaokoa kabisa wao wamjiaro Mungu kwa yeye; maana yu hai sikuzote ili awaombe. **Waebrania 7:25.**

② Yeye awezaye kuwalinda ninyi msjikwae, na kuwasimamisha mbele ya utukufu wake bila mawaa katika furaha kuu. **Yuda 24.**

③ Na kwa kuwa mwenyewe aliteswa alipojaribiwa, aweza kuwasaidia wao wanaojaribiwa. **Waebrania 2:18.**

④ Hata imekuwa, mtu akiwa ndani ya Kristo amekuwa kiumbe kipya; ya kale yamepita; tazama! yamekuwa mapya. **2 Wakorintho 5:17.**

KWA HIYO TUBU

Basi, zamani zile za ujinga Mungu alijifanya kama hazioni; bali sasa anawaagiza watu wote wa kila mahali watubu. **Matendo 17:30.**

Tubuni basi, mrejee, ili dhambi zenu zifutwe, zipate kuja nyakati za kuburudishwa kwa kuwako kwake Bwana. **Matendo 3:19.**

AMINI

Wakamwambia, Mwamini Bwana Yesu, nawe utaokoka pamoja na nyumba yako. **Matendo 16:31.**

UMWUNGAMIE MUNGU DHAMBI ZAKO

Tukiziungama dhambi zetu, Yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu, na kutusafisha na udhalimu wote. **1 Yohana 1:9.**


UMKIRI KRISTO MBELE ZA WATU

Kwa sababu, ukimkiri Yesu kwa kinywa chako ya kuwa ni Bwana, na kuamini moyoni mwako ya kuwa Mungu alimfufua katika wafu, utaokoka. Kwa maana kwa moyo mtu huamini hata kupata haki, na kwa kinywa hukiri hata kupata wokovu. **Warumi 10:9,10.**

Ukitaka kujiunga na mafundisho ya Biblia kwa njia ya Posta tuandikie:

Mambo Manne Ambayo

Mwenyezi Mungu Ataka Uyajue



1 ATAKA UJUE YA KWAMBA UNA HAJA YA KUOKOLEWA.

① Kwa sababu wote wamefanya dhambi, na kupungukiwa na utukufu wa Mungu. **Warumi 3:23.**

② Sisi sote kama kondoo tumepotea; kila mmoja wetu amegeukia njia yake mwenyewe; na Bwana ameweka juu yake Maovu yetu sisi sote. **Isaya 53:6.**

③ Na kama vile watu wanavyowekewa kufa mara moja, na baada ya kufa hukumu.

Waebrania 9:27.

④ Kwa maana mshahara wa dhambi ni mauti; bali karama ya Mungu ni uzima wa milele katika Kristo Yesu Bwana wetu. **Warumi 6:23.**

⑤ Yesu akajibu, akamwambia, Amin, amin, nakuambia, Mtu asipozaliwa mara ya pili, hawezi kuuona ufalme wa Mungu. **Yohana 3:3.**

⑥ Kilichozaliwa kwa mwili ni mwili; na kilichozaliwa kwa Roho ni roho. **Yohana 3:6.**

2 ATAKA UJUE YA KWAMBA HUWEZI KUJIOKOA.

① Iko njia ionekanayo kuwa sawa machoni pa mtu, lakini mwisho wake ni njia za mauti.

Mithali 14:12.

② Hali tukijua ya kuwa mwanadamu hahesabiwi haki kwa matendo ya sheria, bali kwa imani ya Kristo Yesu; sisi tulimwamini Kristo Yesu ili tuhesabiwe haki kwa imani ya Kristo, wala si kwa matendo ya sheria; maana kwa matendo ya sheria hakuna mwenye mwili atakayehesabiwa haki. **Wagalatia 2:16.**

③ Kwa maana mmeokolewa kwa neema, kwa njia ya imani; ambayo hiyo haikutokana na nafsi zenu, ni kipawa cha Mungu; wala si kwa matendo, mtu awaye yote asije akajisifu. **Waefeso 2:8,9.**

④ Yesu akamwambia, Mimi ndimi njia, na kweli, na uzima; mtu haji kwa Baba, ila kwa njia ya mimi.

Yohana 14:6.

⑤ Wala hakuna wokovu katika mwingine awaye yote, kwa maana hapana jina jingine chini ya mbingu walilopewa wanadamu litupasalo sisi kuokolewa kwalo. **Matendo 4:12.**

3 MUNGU AMEKULETEA NJIA YA WOKOVU.

① Kwa kuwa Mungu hakutuweka kwa hasira yake, bali tupate wokovu, kwa Bwana wetu Yesu Kristo; ambaye alikufa kwa ajili yetu, ili tuishi pamoja naye, kwamba twakesha au kwamba twalala.

1 Wathesalonike 5:9,10.

② Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele. **Yohana 3:16**